

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

---

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
ARDHI, MALIASILI NA UTALII

MAONI YA KAMATI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE  
LA KUBADILISHA HADHI MAPORI YA AKIBA YA  
BIHARAMULO BURIGI, KIMISI, IBANDA NA  
RUMANIKA - ORUGUNDU KUWA HIFADHI YA  
TAIFA

*FEBRUARI, 2019*

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(6)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la kubadilisha hadhi ya Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika-Orugundu kuwa hifadhi za Taifa kwa kueleza chimbuko, manufaa na maoni ya Kamati kuhusu uamuzi wa Serikali.

## **2.0 CHIMBUKO LA AZIMIO**

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 16 – 18 Machi, 2018, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilifanya ziara katika Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi kwa lengo la kukagua mradi wa kuyajengea uwezo Mapori ya Akiba kupambana na ujangili. Katika ziara hiyo Kamati ilijiona changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Ubovu wa miundombinu ya barabara ambayo inasababisha sehemu kubwa ya Mapori kutofikika kwa urahisi na hivyo kufanya kazi ya ulinzi kuwa ngumu; na

(ii) Uvamizi wa Mapori uliotokana na uwepo wa wakimbizi kutoka Rwanda uliosababishwa na vita vya mauaji ya Kimbari vya mwaka 1994.

Uwepo wa wakimbizi hao ulisababisha kuongezeka kwa shughuli za binadamu ikiwemo Kilimo, ufugaji, uingizaji wa silaha za kivita uliochangia kuongezeka kwa ujangili.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto hizo zimesababisha maeneo hayo muhimu na yenye

fursa kubwa za Utalii kuharibiwa na kuwa na mchango mdogo kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kubaini changamoto hizo, Kamati iliishauri Serikali kuyapandisha hadhi Mapori hayo kuwa hifadhi za Taifa kwa kuainisha faida za hatua hiyo ambazo ni pamoja na kuimarisha ulinzi wa rasilimali hizo muhimu na kuongeza pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusu kupandisha hadhi Mapori ya Akiba, serikali imeleta hoja ambayo ni Azimio la Bunge. Nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uliamua kuileta hoja hiyo kwenye Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na masharti ya Kanuni ya 53(4) ya Kanuni za Bunge, mapema jana tarehe 8 Februari, 2019, Kamati ilifanyia kazi hoja hii muhimu iliyotokana na ushauri wa Kamati. Kutokana na kazi hiyo, sasa nawasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni na ushauri kwa kuanza na manufaa ya uamuzi.

### 3.0 MANUFAA

**Mheshimiwa Spika**, imeelezwa umuhimu wa kiikolojia wa Mapori hayo ambayo yanapakana na Maziwa, mito, misitu, vijito, maeneo oevu na vyanzo vya maji. Pia, mapori hayo yana miinuko na vilima mbalimbali vinavyopendezesha mandhari ya mapori hayo. Uwepo wa aina mbalimbali za wanyamaporini wakiwemo kuro, viboko, Tembo, Pongo, Ngiri, Fisi, Korongo, Twiga, Swalapala, Nyamela, Tumbili, Mbega mwekundu, Chatu, Pundamilia, Simba na Nyani. Viumbe wengine ni samaki, nyoka, na ndege wa aina mbalimbali. Vile vile Mapori hayo yanapitiwa na mto Kagera na kuna maziwa makubwa ambayo ni Victoria (Biharamulo), Burigi

(Burigi) na Ngoma. Maziwa hayo ni kivutio muhimu cha utalii na ni chanzo cha maji kwa wanyamapor na bioanuai nyingine.

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa Serikali wa kuyapandisha hadhi Mapori hayo ni mwendelezo wa jitihada za Serikali ambapo baada ya kuendesha operesheni ya kuondoa mifugo na wavamizi wengine hali iliyosababisha kuboresha mazingira na sasa wanyamapor waliokuwa wamekimbia wameanza kurejea kwa wingi. Kupandisha hadhi Mapori haya kuwa Hifadhi za Taifa siyo tu kutaimarisha ulinzi bali pia kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hizo na Taifa kwa ujumla. Aidha kuchelewa kupandisha hadhi mapori hayo kutazorotesha jitihada za Serikali za kulinda Maliasili zetu.

**Mheshimiwa Spika**, uwepo wa Uwanja wa ndege wa Chato na kupandishwa hadhi kwa Mapori haya kuwa Hifadhi za Taifa kutachangia sana kufungua fursa za utalii katika Kanda ya Ziwa na hivyo kukuza kipato cha wananchi wanaopakana na hifadhi hizo kutockana na shughuli za utalii.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee Kamati inapenda kumshukuru Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake kwa kukubali ushauri wa Bunge hadi kuwasilisha Azimio la Bunge kwa ajili ya utekelezaji.

#### 4.0 MAONI YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa kupandisha hadhi Mapori haya kuwa Hifadhi za Taifa utaimarisha ulinzi. Hatua hii itajenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la Taifa. Kamati inalishawishi Bunge lako tukufu kuitisha hoja hii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuepusha uwezekano wa hifadhi mpya kukabiliwa na migogoro, Kamati inashauri Serikali kuhakiki Mipaka husika kwa kuwashirikisha wananchi ili kuepuka kuwepo na migogoro ya mipaka.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spka**, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kuchambua Azimio hili na hatimaye kuwasilisha Maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg.Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg,Athman Hussein, Katibu wa Kamati Ndg.Gerald Magili kwa kuratibu shughuli za Kamati.

**Mheshmiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.



Mhe. Kemilembe J. Lwota, Mb  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**  
**ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

9 FEBRUARI, 2019